HOT&TOR – Kiswahili B

T107

Wednesday, 16/11/2016

02:00 – 05:00 PM

WORKFORCE DEVELOPMENT AUTHORITY

P.O. BOX 2707 Kigali, Rwanda Tel: (+250) 255113365

# Mtihani wa Taifa 2016

## Kiswahili B

## Michepuo: HOTELI (HOT) NA UTALII (TOR)

## DURATION: 3hours

**MAELEZO:**

- Mtihani huu ambao una sehemu tatu **I**, **II** na **III**, una maswali 24 lakini utajibu maswali 20 tu kwa alama 100.
- Sehemu ya **I** ina maswali 16 ambapo unapashwa kuyajibu yote kwa alama 55.
- Sehemu ya **II** ina maswali 5 ambapo utajibu maswali 3 tu kwa alama 30.
- Sehemu ya **III** ina maswali 3 ambapo utajibu swali moja tu kwa alama 15.
- Andika vizuri nambari ya kila swali unalolijibu.
- Mwandiko wako usomeke vizuri na ujiepushe na uchafu.
- Tumia kalamu ya bluu au nyeusi.

Siku moja mtoto wa chui alipokuwa akizungukazunguka alijiona amefika mahali ambapo ndovu walikuwa wakilisha. Kusema kweli huyu mwana wa chui alikuwa mdogo sana kwa hivyo hakufahamu kuwa maisha yake yalikuwa yamo hatarini.

Ndovu waliendelea na shughuli yao wala hawakumjali mwana wa chui. Lakini kwa bahati mbaya, bila ya kukusudia, mmoja wao alimkanyaga mtoto wa chui na maskini akafa hapo hapo. Chui waliokuwa wamejificha mtini waliona jinsi mwana wa rafiki yao alivyokufa.Walihuzunika sana, na wakaendelea kuwatazama ndovu jinsi walivyokuwa wakikula nyasi na kukanyaga udongo wakitembea kwa nguvu na malingo. Chui walikaa kimya kwa uoga maana walikuwa wanadhani kwamba huenda ndovu wangewavaamia. Lakini ndovu hawakuwa na nia hiyo. Basi ndovu walipoondoka, chui walimchukua yule mtoto na kumpeleka kwa baba yake.

Alipomuona mwanawe analetwa amekufa mzee chui alijitupa chini akalia kwa uchungu.


"Ni nani huyo aliyeniulia mwanagu? Niambieni nipate kwenda kujilipiza kisasi."

« Ndovu ndio waliomwua, » walijibu rafiki zake.

« Wasemaje, ni ndovu walioniulia kipenzi changu ? » aliuliza mzee chui kwa mastaajabu makubwa. « La, si ndovu waliomwua. Mimi najua ni mbuzi tu walioniulia mwanangu. Ndiyo. Mbuzi ndio waliotenda kisa hiki ! »

Kusema hivi mzee chui alitoka kama mshale na kwa ghadhabu kubwa kabisa akawarukia mbuzi waliokuwa wakilisha milimani na kuwaua wengi wao. Wachache walionusurika walikimbia na kwenda kujificha katika nyumba za binadamu ambazo zilikuwa karibu ya hapo. Waliogopa kwenda mwituni wao wenyewe bila kusindikizwa. Tangu siku hiyo, walianza kuwa chini ya ulinzi mkubwa wa binadmu.

Na mpaka leo mwanadamu anapotendewa mabaya na mtu mwenye nguvu kumshinda yeye hujilipiza kisasi kwa kumwonea mtu aliye mnyonge kuliko yeye. Kweli mnyonge hana haki!



## SEHEMU I: UFAHAMU NA MATUMIZI YA LUGHA — ALAMA 55

(Jibu maswali yote )

**01.** Pendekeza kichwa cha habari hii. **Alama 2**

**02.** Eleza maana ya "kutoka kama mshale" **Alama 2**

**03.** Toa majina mengine ya wanyama wafuatao: **Alama 2**

a. Ndovu: b. Mbogo

**04.** Chui alipokeaje habari ya kifo cha mtoto wake? **Alama 3**

**05.** Kutokana na habari hii, ni mawaidha gani ambayo unaweza kumtolea chui? **Alama 3**

**06.** Unadhani ni kwa sababu gani ndovu amemuua mtoto wa chui? **Alama 3**

**07.** Je, mtoto wa chui alikusudia kuwakaribia ndovu? **Alama 4**

**08.** Chui walipoona mtoto wa rafiki yao ameuawa walikuwa na hisia gani? **Alama 4**

**09.** Je, uoga wa chui ulikuwa na maana? **Alama 4**

**10.** Mnyonge hana haki. Thibitisha ukweli kwa methali hii ukitegemea habari ambayo umeishasoma. **Alama 4**

**11.** Ni kwa nini chui hakwenda kuwatafuta ndovu ili kujilipiza kisasi? **Alama 4**

**12.** Baada ya shida ambayo mbuzi wamepata mwituni wamechukua mikakati gani? **Alama 4**

**13.** Ni shauri gani ambalo unaweza kutolea ndovu? **Alama 4**

**14.** Chagua maneno yanayostahili miongoni mwa haya yafuatayo na kujaza mapengo : tulii, zii, pu, kwikwikwi, lo **Alama 4**

a. Baada ya ajali, Karoli alizimia……
b. Wametukuta tumetulia……
c. Baada ya kifo cha nyanya yake alilia……….
d. Alikuwa amepanda mti na kuanguka……

**15.** Toa maana ya misemo ifuatayo **Alama 4**

a. Kutega masikio:
b. Domo kaya:
c. Kutia masikio pamba:
d. Kukata tamaa:

**16.** Toa methali inayolingana na maelezo yafuatayo: **Alama 4**

a. Usipambane na mtu anayekuzidi nguvu:
b. Mambo yaliyofanywa kwa makini ndiyo yanayofanikiwa:

## SEHEMU II: SARUFI (Chagua maswali matatu ya kujibu) — ALAMA 30

**17.** Jaza nafasi zilizoachiwa wazi ukitumia viunganishi vinavyofaa. **Alama 10**

a. Nitakuandikia …………wewe ni rafiki yangu.
b. Nilikuwa nimechoka……………sasa nimepumzika vya kutosha.

c. Hawajui Kifaransa...............Kiswahili.
d. Nilikuwa nakutafutia mjini ........wewe umeisharudi kijijini!
e. Uliniambia nikununulie nguo...........unajua sina fedha.

**18.** Chagua neno sahihi. **Alama 10**

a. Uwera alifanya kazi (taratibu/haraka) akachelewa.
b. Majirani walilia kwa (shangwe/huzuni) baba alipofariki.
c. Babu anazungumza (taratibu/upesi) na kwa makini.
d. Chakula hiki ni (kingi/kidogo) hakitoshi.
e. Gari lilienda (kasi/taratibu) na kupindukia.

**19.** Unda sentensi kutokana na jedwali lifuatalo **Alama 10**

| Nomino | Kivumishi | Kitenzi |
|---|---|---|
| Samaki | | |
| Mswaki | | |
| Ugonjwa | | |
| Vidole | | |
| Mpapai | | |

**20.** Tumia maneno badala ya tarakimu na kujaza mapengo. **Alama 10**

Mfano. Watu 2 ---tembea. Watu

a. Mbogo 12 waliwindwa.
b. Marais 4 waliungana.
c. Nge 3 ---lituuma.
d. Nyoka 7---metushambulia.
e. Kidole 1 ha----vunji chawa.

**21.** Unganisha tungo mbili ziwe moja ukitumia kiambishi “vyo” cha jinsi. **Alama 10**

a. Fundi anashona. Mimi ninashona kama yeye.
b. Mwalimu alisimama. Sisi tulisimama kama yeye.
c. Mlipendekeza tufanye kazi. Tulifanya hivyo.
d. Niliambiwa kuandika vizuri. Nilivifanya.
e. Watatuomba kucheza. Tutafanya hivyo.

**SEHEMU III: UTUNGAJI** (Jibu swali moja) **ALAMA 15**

**22.** Fupisha habari ambayo umeishasoma hapo juu kwa theluthi moja. **Alama 15**

**23.** Tunga insha kati ya mistari kumi na kumi na mitano kuhusu sherehe za kuanza mwaka mpya. **Alama 15**

**24.** Tunga hadithi simulizi yenye mistari kati ya kumi na mitano na ishirini. **Alama 15**